TANGAZO LA SERIKALI NA. 156 la tarehe 3/3/2023

SHERIA YA HUDUMA ZA MASHTAKA YA TAIFA,

(SURA YA 430)

# NOTISI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 22)*

NOTISI YA UTEUZI WA WAENDESHA MASHTAKA YA MWAKA 2023

Jina

1. Notisi hii itajulikana kama Notisi ya Uteuzi wa Waendesha Mashtaka ya Mwaka 2023.

Uteuzi wa waendesha mashtaka

2. Watu ambao majina yao yameorodheshwa katika Jedwali wanateuliwa kuwa waendesha mashtaka kwa madhumuni ya kuendesha kesi za jinai kwa niaba ya Mkurugenzi wa Mashtaka.

Uhalali wa uteuzi

3.-(1) Mwendesha mashtaka aliyeteuliwa chini ya aya ya 2 atatumikia nafasi hiyo kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia tarehe ya kuanza kutumika kwa Notisi hii.

(2) Bila kujali aya ndogo ya (1), mwendesha mashtaka aliyeteuliwa chini ya Notisi hii anaweza kuendesha mashtaka kwa kipindi kinachopungua miaka mitano pale ambapo ajira ya mtu huyo katika utumishi wa umma itakoma au uteuzi wake utasitishwa na Mkurugenzi wa Mashtaka.

*Tangazo la Serikali na. 156 (linaendelea)*

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

| Na. | Jina |
|---|---|
| 1. | PF. 21127 A/Insp. Witness Bura |
| 2. | G. 5229 Cpl Renifrid William |
| 3. | A/Insp. Mweta Samweli |
| 4. | Hamis Y. Mattaka |

Dodoma,
22 Februari, 2023

SYLVESTER ANTHONY MWAKITALU,
*Mkurugenzi wa Mashtaka*